**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU- TAMISEMI**

---


Namba za simu:
**Mkuu wa shule**: 0715333956
**Makamu Mkuu wa Shule**: 0626817194
**Bording Master:** 0688724612

Shule ya Sekondari Mwenge,
S.L.P 195,
**SINGIDA.**


Tarehe……………………….

**Jina la mwanafunzi,**

………………………………………..
S.L.P ………………………………....
………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWENGE ILIYOPO HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA MKOA WA SINGIDA KWA MWAKA WA MASOMO………………...**

## 1. UTANGULIZI

Napenda kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha……katika shule ya Sekondari **MWENGE**. Uongozi wa shule tunakupa hongera sana kwa kufaulu mtihani wa kidato cha nne na kufaulu kwa Daraja zuri ambalo limekuwezesha kujiunga na masomo ya kidato cha………..

Shule ya sekondari **MWENGE** ni shule inayochukua wanafunzi wavulana wa kidato cha……………… Tunakukaribisha sana katika shule yetu ili upate elimu bora kwa maslahi mapana ya kwako, familia na Taifa kwa ujumla. ***Tunakukumbusha kuwa kwa sasa ndio umeianza rasmi safari yako ya kutengeneza maisha yako kwa elimu utakayoipata hapa Mwenge, kwa hiyo ni muhimu sana kuwa mtulivu na kuitumia nafasi hii uliyoipata vizuri.***

Aidha, maelezo yaliyotolewa hapa kweye fomu hii yasome vizuri na kuyaelewa.

### 1.1 KAULI MBIU, DIRA, DHAMIRA NA WIMBO WA SHULE

#### 1.1.1 KAULI MBIU (MOTTO):

Mwenge Secondary School shall perpetuate Work, Educational and Discipline of students

#### 1.1.2 DIRA (VISION):

Mwenge Secondary School to excel academically and culturally for national development **[Dumisha Kazi, Elimu na Nidhamu]**

#### 1.1.3 DHAMIRA (MISSION):

Mwenge Secondary School shall strive to

(i) Attract quality staff
(ii) Discipline students
(iii) Provide adequate teaching/learning materials
(iv) Create an enabling environment for academic excellency
(v) Creating and strengthening partnership/collaboration with others

#### 1.1.4 WIMBO WA SHULE:

Msingi imara tena wa kweli,
Umekwisha wekwa na shule yetu,
Taluma michezo na pia umoja,
Usafi na nidhamu ni sifa zetu,
***Chorus Mwenge shule yangu ninakupenda !***

## 2. MASOMO YANAYOFUNDISHWA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MWENGE

Shule ya sekondari Mwenge ina michepuo ya **sayansi na sanaa**, kwa upande wa sayansi, michepuo ni **PCB, PCM, CBG, PMCs, na EGM** na kwa upande wa sanaa michepuo ni **HGE, HGL, HGK, na HKL.** Kwa kuzingatia michepuo hiyo masomo yanayofundishwa ni Physics, Chemistry, Biology, Advanced Mathematics, Geography, Computer Science, Economics, History, English Language, na Kiswahili

## 3. MAHALI SHULE YA SEKONDARI MWENGE ILIPO

Shule ya seKondari Mwenge ipo Singida mjini kilometa moja na nusu (1.5) kaskazini kutoka stendi kuu ya mabasi **"Misuna Bus TerminaL"**. Usafiri kutoka stendi hadi

shuleni ni wa bajaji/pikipiki. Nauli ni shilingi 1,000/= kwa bajaji na 1,000/=kwa pikipiki usafiri huu unapatikana katika kituo cha mabasi "Misuna Bus Terminal".

**4. KUFUNGUA SHULE**

Muhula wa masomo unaanza tarehe Itakayotangazwa na Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe iliyotajwa ya kufungua shule bila kuchelewa.

**5. OFISI UTAKAZOPOKELEWA MARA TU UNAPOINGIA ENEO LA SHULE**

Ukifika shuleni nenda moja kwa moja ofisi ya **MKUU WA SHULE** kwa ajili ya maelekezo na kupewa utaratibu wa usajili. **Muda wa usajili ni kuanzia saa 1:300 asubuhi hadi saa 12:00 jioni.**

**6. MAHITAJI YA SHULE KWA MWANAFUNZI ANAYEJIUNGA KIDATO CHA TANO**

**6.1 MICHANGO YA SHULE**

Fedha za michango zilipwe kwenye Akaunti ya shule **Na 50801100022** katika Benki ya NMB jina la akaunti ni ***Mwenge Secondary Education Development.*** Kabidhi bank pay in slip halisi kwa mhasibu na ubaki na nakala yako kwa kumbukumbu.

| Na | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho | 5,000/= |
| | **JUMLA YA MICHANGO YOTE NI: -** | **80,000/=** |

**6.2 BIMA YA AFYA**

***Kila mwanafunzi aje na bima ya afya***. Ndugu mzazi/mlezi kama mwanao hana bima ya afya unatakiwa umkatie bima ya afya ya Tsh 50,400/= kwenye Hospitali iliyokaribu nawe au unaweza kuja na fedha tajwa hapo juu ili uongozi wa shule ufanye utaratibu wa kumkatia bima yake ya afya. **SHULE HAINA GHARAMA ZA MATIBABU KWA WANAFUNZI KWANI HILO NI JUKUMU LA MZAZI/MLEZI.**

## 6.3 VIFAA VYA TAALUMA KWA MWANAFUNZI

(i) Rimu mbili (2) A4 aina ya Double A kwa kila mwaka. Rimu moja (1) atakabidhi siku ya usajili na itakayobaki atakabidhiwa kwa ajili ya mazoezi ya walimu.

(ii) Dissecting tray kwa wanafunzi Wote wa mchepuo wa sayansi.

(iii) Jalada au file jipya (spring file) kwa wanafunzi wote na utalikabidhi siku ya usajili kwa ajili ya kuwekea kumbukumbu zako za kishule

(iv) Scientific calculator – function 991 kwa wanafunzi wa michepuo ya sayansi na HGE. Atakaguliwa na atarudishiwa kwa ajili ya matumizi yake ya darasani.

(v) Stop watch kwa wanafunzi wote wa sayansi.

(vi) Madaftari ya kutosha Q3 yasiyopungua kumi (10) kwa kila mwanafunzi.

(vii) Begi la kubebea madaftari wakati wa masomo kwa wanafunzi wote.

(viii) Kalamu, penseli, vifuto, rula. (aje navyo vya kutosha).

(ix) Mzazi/Mlezi unapaswa kumnunulia mwanao vitabu vyake vya kujisomea. Angalia list iliyoambatanishwa kwa kila somo.

## 6.4 MAHITAJI YA BWENINI KWA WANAFUNZI WOTE

(i) Godoro lenye foronya la (upana futi 2½ ujazo inchi 3 na urefu futi 6)

(ii) Chandarua chenye rangi ya bluu

(iii) Tranka kubwa lenye sehemu za kuwekea kufuli mbili kwa usalama wa vifaa vyake.

(iv) Mfungulie mwanao akaunt ya CRDB, NMB, NBC, DTB au TPB kwani hizi benki zinapatikana kwa urahisi hapa shuleni. Shule haitahusika na upotevu wa fedha bwenini. Kwa msaada zaidi anaweza kufungua akaunti yake ya bank akiwa hapa shuleni kwani siku za usajili bank zote hutumia nafasi hiyo kuwafungulia wanafunzi akaunti zao.

(v) Utalala kwenye bweni ulilopangiwa tu, hairuhusiwi kuingia kwenye bweni ambalo hujapangiwa.

(vi) Aje na Yebo za heshima rangi nyeusi au malapa rangi yeyote kwa matumizi ya bwenini na siku za wikendi.

(vii) Tochi ndogo inayoweza kumsaidia nyakati za usiku.

(viii) Bakuli la chakula na lenye sehemu ya kuwekea mboga

(ix) Kikombe cha uji

(x) Kijiko cha kulia chakula

## 6.5 SARE YA SHULE

Shule hii ni ya **Bweni** na ni ya **Wavulana pekee** hivyo sare ya shule ni:-

(i) Shati mbili nyeupe za tetroni mikono mirefu.

(ii) Suruali mbili za rangi ya **"Jungle green"** na **Isiwe Green**, Suruali hizi zishonwe bila kuwekewa Marinda, pia isiwe ya kubana wala mdomo wa chupa miguuni. **Angalia kiambatanisho "D"**

(iii) Mwanafunzi aje na sweta, T-shirt na Tai 2, muonekano wa sare hizo ni kama ulivyo kwenye **kiambatanisho "D"**

(iv) Nguo za kushindia (shamba dress) ni suruali mbili za kitambaa cha Khaki. Endapo mzazi atapata tatizo la kupata sare za shule kutokana na changamoto ya mazingira alipo anaweza kuzipata katika duka lililoko karibu na shule kwa mchanganuo ufuatao:- T- shirt yenye nembo ya shule 15,000/=, Sweta rangi ya jungle green 15,000/=, Tai Mbili 8,000/= Suruali ya Jungle Green (kitambaa namba moja) 25,000/= Suruali Rangi ya kaki 20,000/=.

(v) Viatu vyeusi vya kufunga na Kamba na vyenye visigino vifupi

(vi) Soksi jozi mbili nyeusi za kuvalia na viatau vya shule

(vii) Mkanda mweusi wa Ngozi wa kuvalia suruali

(viii) Viatu vya michezo aina ya njumu(six) rangi yeyote na Soksi

(ix) Mwanafunzi aje na jezi moja ya michezo yaani bukta na "T-shirt'' (Tzs 12,000/=) kwa mchanganuo ufuatao:

| | |
|---|---|
| HGL | - Jezi nyeusi mistari myeupe |
| HGK | - Jezi ya rangi ya chungwa mistari myeusi |
| HGE | - Jezi kijani ya jeshi mistari ya njano |
| HKL | -Jezi nyeusi mistari myekundu |
| EGM | -Jezi ya zambarau mistari myeupe |
| CBG | - Jezi nyeusi mistari ya njano |
| PCB | -Jezi nyekundu mistari myeupe |
| PCM | -Jezi ya bluu mistari ya njano/myeupe |
| PMCs | -Jezi nyeupe mistari myeusi |

**ZINGATIA:** Mwanafunzi haruhusiwi kufika shuleni na nguo nyingine yoyote tofauti na hizo alizoagizwa kwenye barua ya maelekezo. **Mwanafunzi afike shuleni akiwa amevaa suruali ya khaki na shati nyeupe ya mikono mirefu**

### 6.6 VIFAA VYA USAFI KWA TAHASUSI ZOTE

(i) **CBG, PCM** na **PCB** – Sabuni ya maji(careline ya kijani) lita 5(galoni 1), Rubber squizeer 1, Chelewa 1 na ndoo ndogo mbili(2)

(ii) **PMCs** – Brash za kusugulia masinki ya chooni 2, chelewa mbili (2) jembe, rubber squizer 1 na ndoo ndogo mbili (2).

(iii) **EGM** na **HGE** -Soft broom mbili (2), Aro moja(1), chelewa moja (1), rubber squizer moja (1), ndoo kubwa moja (1) na ndoo ndogo moja (1).

(iv) **HGL-** Brashi mbili (2) za kusugulia masinki ya chooni, rubber squizer moja 1, jembe na mpini wake moja (1), chelewa mbili (2) na ndoo ndogo mbili (2).

(v) **HKL**- Mkasi mkubwa wa kukatia maua mmoja(1), chelewa moja(1) na ndoo ndogo mbili (2).

(vi) **HGK**-Shoka na mpini wake moja (1), moper moja (1), chelewa moja (1) na ndoo ndogo mbili (1).

## 7. TAALUMA KWA MWANAFUNZI

Kama ilivyo shule zingine hapa nchini, Shule ya sekondari Mwenge inajali sana taaluma ya mwanafunzi kwa manufaa ya taifa letu. Hivyo basi kwa kuzingatia hilo mwanafunzi anapaswa kuwepo kila wakati katika maeneo ya taaluma yafuatayo:-

(i) Ahudhurie darasani siku zote za masomo kama ilivyoainishwa kwenye kalenda ya masomo. Kukosa kipindi bila sababu ni hatari kubwa kwako ikiwemo na kuchukuliwa hatua.

(ii) Kufanya kazi zote za walimu za siku husika bila kukosa, tena kwa welendi wa kutosha na sio kubahatisha.

(iii) Kufuata ratiba ya shule

(iv) Kuingia kwenye preparation za usiku (prepo) bila kukosa. Mwanafunzi atakaekosa siku mbili mfululizo atachukuliwa hatua.

(v) Kufanya mitihani yote utakavyoelekezwa na walimu wako.

(vi) Utahudhuria vipindi vya dini siku ya ijumaa bila kukosa

## 8. HESHIMA, ADABU NA UTII KWA WANAFUNZI WOTE WA MWENGE SEKONDARI

### 8.1 HESHIMA, ADABU NA UTII

Mwanafunzi aliyechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Mwenge hana budi kuwa na adabu, utii na heshima kwa walimu wake, watumishi

wengine, wanafunzi wenzake na jamii kwa ujumla. Mwanafunzi atakayebainika kutokuwa na tabia njema au kuwa jeuri **ATAFUKUZWA SHULE MARA MOJA.** Aidha mzazi anatakiwa amwonye mwanae na kumtahadharisha na tabia za kutofuata sheria za shule.

## 8.2 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

(i) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule

(ii) Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (preparation)

(iii) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa

(iv) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii

(v) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule

(vi) Kuvaa sare ya shule wakati wote kulingana na maelekezo ya shule.

(vii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

(viii) Kutunza mali za shule

(ix) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya Mwalimu/daktari

(x) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

## 8.3 MAKOSA MENGINE YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI AFUKUZWE SHULE MARA MOJA BILA KUCHELEWA

(i) Wizi

(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku **90** bila taarifa/utoro

(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo

(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla

(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga Mwalimu au mtu yeyote yule

(vi) Kunyoa nywele kwa mtindo usiokubalika na kufuga ndefu. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wawapo shuleni, huduma ya kunyoa inapatikana shuleni

(vii) Ulevi au unywaji pombe na matumizi ya madawa ya kulevya

(viii) Uvutaji wa sigara

(ix) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa
(x) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
(xi) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
(xii) Kumiliki kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
(xiii) Kudharau bendera ya Taifa
(xiv) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
(xv) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi
(xvi) Kusiriki matendo ya uhalifu, uchohezi wa kisiasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
(xvii Kutoka nje ya shule bila ruhusa ya Mwalimu

**MUHIMU:**

(a) Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shule kwa namna yoote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.
(b) Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu
(c) Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum kutoka kwa mkuu wa shule. (msiba au ugonjwa).

**9. VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU**

(a) Fomu ya uchungunzi wa afya (medical Examination form) ambayo itajazwa na mganga wa hosipitali ya serikali
(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanfunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa michango na kutekeleza maelekezo mengine yatakayotolewa na shule
(d) Picha (passport size) nne (4), mbili za wazazi/walezi yaani moja moja na mbili za ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni Pamoja na namba zao za simu

**10.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu, mwanfunzi atasajiliwa tu baada ya kutekeleza maagizo haya na kukabidhi fomu zilizojazwa kikamilifu na si vinginevyo.



KARIBU KATIKA SHULE HII,

……………………………………..

**METHODI T. NJIKU**
**MKUU WA SHULE**
**0715333956**

**NB:- Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi unatakiwa utume pesa, TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO**: -Mkuu wa Shule 0715333956/0784269211

**KIAMBATANISHO A.**

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWENGE**

**A: SEHEMU YA MWANAFUNZI**
**MWANAFUNZI AJAZE SEHEMU HII.**

1. Mimi ................................................................. ninakubali kujiunga na shule ya sekondari mwege kidato cha .................. kwa machaguo ya (combination) ................
2. Mimi ni mwanafunzi wa Mwenge sekondari, ninakubali kwamba:
   (i) Nitafika shuleni siku ya kufungua na bila kuchelewa kila muhula
   (ii) Nitatii sheria za shule Pamoja na kutoshiriki katika ulevi, migomo na migogoro ya aina yeyote
   (iii) Sitaleta shuleni wala kuvaa mavazi yasiyo ya heshima kama nguo za kubana, kofia miwani ya giza, pete za urembo
   (iv) Nitatumia juhudi na maarifa yote kujiimarisha kitaaluma ikiwa ni Pamoja na kuhudhuria vipindi na kufanya mazoezi na mitihani yote (k.v. usafi na elimu ya kujitegemea.

Saini ya mwanafunzi ……………………………….. Tarehe ……………………………

**B. SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**
**MZAZI/MLEZI AJAZE SEHEMU HII**

Mimi ………………………………………nimekubali mtoto wangu …………………………

Ajiunge na shule ya sekondari Mwenge kuanzia tarehe …………………………………

1. Mimi .................................................nimekubali mtoto wangu .................................... ajiunge na shule ya sekondari Mwenge kuanzia tarehe .......................................

(i) Nitawasaidia walimu kumlea mwanangu kitaaluma na kitabia. Nitamuonya na kumsisitiza mwanangu kutii sheria zote za shule na kuishi maisha mazuri kwa maadili ya kiuanafunzi

(ii) Nitamkataza kuvaa nguo zisizo za heshima kama nguo za kubana, kofia, miwani ya giza n.k

(iii) Nitampatia mtoto wangu nauli ya kuja shuleni na kurudi likizo bila kuchelewa

(iv) Nitahakikisha anakuja shuleni siku ya kufungua kila muhula bila kuchelewa

Anwani yangu ya kudumu ……………………………………………………………………….
Sahihi ya Mzazi/Mlezi ………………………………………….. Tarehe ………………………..

***(Tafadhali njoo na fomu hii unapokuja shuleni ikiwa imejazwa).***

**Kiambatanisho B.**

**FOMU YA MAELEZEO BAYANA (PERSONAL PARTICULARS)**

**KWA AJILII YA USAJILI IJAZWE NA MZAZI/MLEZI.**

1. Jina kamili la mwanafunzi kama alivyoandikisha kwenye mtihani wa kidato cha nne ………………………………………………………………
2. Jina kamili la Baba/Mlezi ………………………………………………………………

   (a) Anwani ya Baba/Mlezi ………………………………………………………………

   (i) Namba ya simu ya Baba/mlezi kazini ……………………………………Nyumbani ……………………………………………………………………………

   (ii) Mtaa/Kijiji ………………………………… Kata ………………………… Tarafa ……………………… Wilaya ……………………………………………………… anakokaa
3. Jina la Mama/Mlezi ………………………………………………………………………

   (i) Anwani ya Mama/Mlezi ………………………………………………………………

   (ii) Namba ya simu ya Mama/Mlezi ……………………………………………Nyumbani ……………………………………………………………………………

   (iii) Mtaa/Kijiji ………………………… kata ………………… Tarafa……………………… Wilaya ……………………………………………… anakotoka
4. Tarehe ya kuzaliwa mwanafunzi ………………………………………………………………………
5. Mahali alipozaliwa ……………………………………… Mkoa ……………………………………… Wilaya………………………………… Kijiji/Mtaa
6. Kazi ya Baba/Mlezi ………………………………………………………………………………………
7. Kazi ya Mama/Mlezi ………………………………………………………………………………………
8. Je mwanafunzi anacho kilema chochote? ……………………………………………………… kijaze ………………………………………………………………………………………………………
9. Taja ndugu watatu ambao wanaweza kutoa msaada kwa mwanao.

| NO | JINA KAMILI | KAZI | UHUSIANO | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |

**TAREHE …………………………………………… SAHIHI YA MZAZI/MLEZI …………………**

**KIAMBATANISHO C**

MWENGE SECONDARY SCHOOL,

S.L.P 195,

**SINDIDA**

To: The Medical Officer

……………………………………

……………………………………

……………………………………

Dear Sir/Madam

**REF: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please examine Mr/Miss ……………………………………………………as to his/her fitness as a full -time advanced level of Secondary education studies. My I kindly request you to fill in the particulars given in the form here under.

Yours Sincerely

………………………………

The headmaster

**TO BE COMPLETED BY THE MEDICAL OFFICER**

1. Blood count (white blood cells) ..................................................................................
2. Stool examination ......................................................................................................
3. Urine examination ......................................................................................................
4. Eyesight .......................................................................................................................
5. Hearing ........................................................................................................................
6. Venereal diseases .......................................................................................................
7. T.B test ........................................................................................................................
8. Chest ...........................................................................................................................
9. Does he/she has any chronic disease for epilepsy cell, Anemia, Athma etc ......................................................................................................................................

I have examined the above – named and consider that he/she physically fit/ unfit and mentally fit/ unfit for a full – time advanced lever of Secondary education studies.

Date ……………………………………………………… Signature ………………………….

Station …………………………………………………… Designation ……………………….

KIAMBATANISHO D





# ORODHA YA VITABU VYA MASOMO.

## VITABU VYA HISTORIA

## READING LIST FOR HISTORY ONE


1. Webster J.B The Growth of African Civilization, the Revolutionary years of West Africa since
   1800, Longman Press
2. Walter Rodney, How Europe Underdeveloped Africa.
3. Hallert, R. (1983). Africa since 1875 vol 3 East Africa Educational Publishers Nairob, Kenya.
4. July, R.W. (1992). A History of the African people, East African Educational publishers, Nairobi, Kenya
5. I life, J. (1995). Africans, the history of the Continent. Edinburg, Cambridge, University Press, London UK
6. Maning P, (1990). Slavery and African life; Occidental Oriental and African slave trad, Cambridge University Press.
7. Njiro, E. (1989). A History of African in the 19th century. Literature Bureau Nairobi, Kenya
8. Rodney, W. (1976). How Europe underdeveloped Africa, publishing House Dar-es-salaam, Tanzania
9. Shillington, K. (2004). History of Africa, Macmillan Publishers. Hong Kong, Japan.
10. Davidson, E. EFAL (1997) The growth of the African civilization East and central Africa to the late 19th century, Longman Group Limited, Singapore
11. Freud, B. (1998) The making contemporary Africa, The Development of Africa societies
    since 1800, Colorado, Lynne Reiner publisher
12. Kimambo, I and Temu, A (1969), A history of Tanzania, East Africa Publishing House Nairobi, Kenya.
13. Robin, H. (1993), African since 1875 A modern History, East African Publishers Ltd Nairobi, Kenya
14. Roland O. And Anthony, A (2007). Africa since 1800 A Cambridge University Press New York,
    USA
15. History for secondary school form five (Tanzania Institute of Education)
16. History for secondary school form six (Tanzania Institute of Education)
17. History for secondary school, Form five (TIE)
18. History for secondary schools, form six (TIE)


#### READING LIST FOR HISTORY TWO


19. Nelson throne modern word history
20. History of 21st century (World history) OXFORD
21. H.L Peacock, A history of Modert Europe 1789-1981 seventh Edition (2010)
22. The history of Modern World (2007) 6th Edition by Oxford University Press.

**b) VITABU VYA KISWAHILI**

1. J.A. Masebo na M.NYangwine, Nadharia ya Kiswahili kidato cha tano na sita
2. H.J Mwasiko, R.D.K.Mekacha, D,L.Masoko, P.C.K.Mtengwa; Kitangulizi cha Tafsiri Nadharia na mbinu
3. Tahakiki kidato cha tano na sita
4. Nadharia ya fasihi kidato cha tano na sita Kiswahili II
5. Kiswahili 1 Mwandishi Masuko Chistopher Saluhaya.
6. Kitangulizi cha Tafsiri, Nadharia na Mbinu waandishi H.J.M.Mwansoko
7. Kiswahili sekondari -Kidato cha Tano (TIE)
8. Kiswahili Sekondari -Kidato cha sita (TIE)

**(C)VITABU VYA JIOGRAFIA**

1. Pritchard J.M.(1979), Africa a study Geography for Advanced students London Longman
2. Msabila D.T (2003) Success in Geography climatology and soil Science Dar-es salaam – Afroplus Industries L.T.D
3. Prichard J.M (1990) practice Geography Africa, Longman
4. Kamili A comprehensive Approach Practical Geography for Advanced level, Dar-es-salaam, Afroplus Industries
5. Kamili, physical Geography for Africa, Dar-es-salaam Afroplus Industries
6. Msabila D.T. Physical Geography, Dar-es-salaam Nyambari Nyangwine Publisher
7. Msabila D.T. (2006) Human and economic Geography (Advanced level paper 2) Nyambari Nyangwine publisher

(**d) VITABU VYA LANGUAGE (1) ONE**

1. Nicholus arshery, Comprehensive English Grammar New edition
2. Michael kadeghe, sematics photology and styhstics. (blue)
3. Ashel, N. (2009) Advanced level English A practical Approach DSM
4. Kandeghe, Michael (2011) The real Englis textbook for Advanced level (form five) DSM
5. English language for secondary school language & usage – form fice & six (TIE) Papers
6. Advanced English language: form five & six by Oxford

**(e) LANGUAGE (II)**

1. Ashel, N, (2011), Advanced level literature. The Essential Guide; Good book publisher DSM

2. Advanced level Literature, (2008), Nyambari Nyangwine publisher, DSM
3. Achebe A, (1996) A man of the people
4. AYI Kwei Arman (1968), The Beautiful Ones Are Not Yet Born
5. Ibsen, H, (1882) An enemy of the people, EA- DSM
6. Imbunga, FC (1976) betrayal in the city
7. Mirii Ngui& Thing'ol (1982), I will Mary when I want, EAEP, DSM
8. Institute of Education, selected poems
9. Mloka, C. (2007) The wonderful surgeon
10. English language for secondary school, literature & stylistics – form five & six (TIE) paper 2

(f) **GENERAL STUDIES: -**

1. General studies Approach
2. Richard, R.F.Mbalase, General studies for Advanced level 3rd Ed
3. Mgaywa, B.M General Studies for Advanced level 3 rd Ed
4. Joannes Bigirwa Mungu& Sospeter. M. Deogratias. Understanding Advanced lever general studies; Advance secondary school Education.

**(g) VITABU VYA FIZIKIA**

1. S.Chand – Conceptual physics XI na XI
2. Nelkond and Parker Physics
3. Ransden physics.

**(b) VITABU VYA KEMIA**

1. By S.Chand, conceptual Chemistry for class X and XIII
2. By Tanzania Institute of Education, Advanced Level In Organic Chemistry part I and II
3. Advanced chemistry review (2000-2012) 4. Ramsden, E.M (2000) A-Level Chemistry 4th Edition II

**(c) VITABU VYA BIOLOJIA**

1. By Tayloratel (1999) Biological Science, third edition by C.J.Tranter
2. Pure mathematics, by J.K Backhouse
3. Engineering Mathematics sixth edition by K.A STROUD
4. Advanced Mathematics 1-review (problems & solutions)

**(k) BASIC APLLIED MATHEMATICS**

1. Additional and Applied Mathematics by J.F.TALBERT
2. Basic applied mathematics (BAM) by Respicius kiiza and Lugano Mwanginde
3. basic applied mathematics review questions and solution.